JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO

## UINGIZAJI WA MASUALA JINSIA KATIKA UFUATILIAJI NA TATHMINI ZA SHUGHULI ZA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI ILIYOWASILISHWA KWA BODI YA TAIFA YA URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI KWENYE UKUMBI WA CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI SINGIDA

**TAREHE 01 JULAI, 2009**

**Imeandaliwa na Kuwasilishwa na;**
**Julius Mbilinyi**
**Idara ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali,**
**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**
**S.L.B. 3448, DAR-ES-SALAAM**

# 1.0. Utangulizi

- Katika miaka ya hivi karibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) yanatambulika kuwa ni wadau muhimu katika Maendeleo ya Jamii na Taifa kwaujumla.

- Kumekuwepo na jitihada za kutambua na kubainisha mchango wa Mashirika haya.

- Vyombo mbalimbali vimeundwa kisheria ili kufanikisha azma hiyo ikiwa ni pamoja na Bodi ya Taifa ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Idara ya Uratibu ya Uratibu wa Mashirika haya yenye Sehemu ya Ufuatiliaji wa Shughuli za NGOs.

- Mada hii ya Uingizaji wa Masuala ya Jinsia katika Ufuatiliaji na Tathmini ya Shughuli za NGOs katika kubaini mchango wa Mashirika haya ina sehemu kuu saba ambazo ni:-

❖ Utangulizi;
❖ Tafsiri ya Dhana Mbalimbali;
❖ Umuhimu na Sababu za Kuingiza masuala ya Jinsia katika Ufuatiliaji na Tathmini za shughuli za NGOs;
❖ Hatua za kuingiza masuala ya Jinsia katika Ufuatiliaji na Tathmini ya shughuli za NGOs;
❖ Umuhimu wa Bajeti na Kaguzi zenye mtazamo wa Kijinsia katika Ufuatiliaji na Tathmini ya shughuli za NGOs;
❖ Hitimisho;
❖ Mapendekezo

# 2.0. Tafsiri ya Dhana Mbalimbali

Dhana kuu katika Mada hii ni Jinsia *(Gender),* Uingizaji wa masuala ya Jinsia *(Gender mainstreaming*) na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

**Jinsia** ni mahusiano baina ya wanawake na wanaume, wasichana na wavulana ambayo hujengwa kulingana na tamaduni za jamii husika katika muda husika.

**Uingizaji wa masuala ya Jinsia** ni dhana inayosisitiza umuhimu wa kuzingatia mahitaji na maoni ya wanaume na wanawake, wasichana na wavulana katika mipango mbalimbali, utekelezaji,ufuatiliaji na tathmini za maendeleo. Kwa maneno mengine uingizaji wa masuala ya Jinsia katika ufuatiliaji na Tathmini za shughuli za NGOs ni moja ya mikakati ya kufikia usawa wa Kijinsia.

**Mashirika Yasiyo ya Kiserikali** yanatafsiriwa kuwa ni vikundi vya watu au mashirika huru yaliyoungana katika ngazi ya Wilaya, Mkoa, Taifa na Kimataifa ili kuleta maendeleo halali ya kijamii na kiutamaduni au kulinda mazingira au kutetea maslahi ya umma au kikundi cha watu pasipo kugawana faida; na yanajumuisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyoanzishwa chini ya mwamvuli wa Mashirika ya Dini au Mashirika ya kueneza imani au Chama cha Wafanyakazi, Klabu ya Michezo, Chama cha Siasa au Kikundi cha Kijamii **LAKINI** hayajumuishi Vyama vya Wafanyakazi, Klabu za Michezo, Vyama vya Siasa, Vikundi vya Kijamii au Mashirika ya Dini.

# 3.0 Umuhimu na Sababu za Kuingiza masuala ya Jinsia katika Ufuatiliaji na Tathmini za Shughuli za NGOs

Uingizaji wa masuala ya Jinsia unaboresha matumizi ya Bajeti unaongoza uwazi na uwajibikaji. Pia ni mfumo jumuishi ambao huboresha ushiriki na umiliki wa Mipango na Utekelezaji kwa Makundi mbalimbali katika jamii. Hivyo Sera, Mikakati na Sheria mbalimbali zinaweka msisitizo katika kuingiza masuala ya Kijinsia kama inavyoainishwa kwa baadhi ya Sera zifuatazo:

(i) Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Jinsia na Wanawake (2000) na Mpango wake mkakati vinatoa mwongozo wa kuingiza masuala ya Jinsia katika Mipango mbalimbali na mchakato mzima wa maendeleo.

(ii) MKUKUTA unaainisha Jinsia kama moja ya masuala mtambuka. Hivyo unaelekeza Sekta na idara mbalimbali kuingiza masuala ya Jinsia kwenye mipango yao yote kama suala mtambuka. Aidha MKUKUTA unaweka viashira kwa ajili ya kufikia usawa wa Kijinsia na kujenga uwezo wa wanawake.

(iii) Mikataba na Malengo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kama vile, CEDAW, Azimio la Beijing, Azimio la Jinsia na Maendleo ya SADC, Azimio la Maputo la 50/50 vitafikiwa na kutekelezwa ikiwa masuala ya Kijinsia yataingizwa katika mipango mbalimbali ya maendeleo kama vile kufuatilia na kutathmini shughuliz a NGOs.

(iv) Aidha Sera mbalimbali ikiwemo Sera ya Taifa ya Nje zinatambua ushiriki wa Mashirika haya kupitia shughuli zake hutoa mchango mkubwa wa maendeleo ya makundi mbalimbali katika jamii ikiwemo wanawake na wanaume.

# 4.0 Hatua za Kuzingatia katika Kuingiza masuala ya Jinsia katika Ufuatiliaji na Tathmini za Shughuli za NGOs

- Uingizaji wa masuala ya Jinsia siyo Mipango na Bajeti mpya bali ni Mipango na Bajeti jumuishi yenye mtazamo wa Kijinsia *(Gender Perspective).* Kuna hatua mbalimbali za kuzingatia katika kuingiza masuala ya Kijinsia katika Ufuatiliaji na Tathmini za shughuli za NGOs nchini. Aidha hatua hizi kama njia ya kufikia usawa wa Kijinsia hutumia pia mikakati mitatu ya kufikia usawa wa Kijinsia ambayo ni Ujumuishi, Mageuzi ya kutoa usawa katika kuthaminisha michango ya wanaume na wanawake na kufanya mabadiliko katika mfumo wa Kijinsia kwa mfano kuufanya uwe rafiki kwa malezi ya watoto. Hatua hizi ni kama zifuatazo:

**(i) Uchambuzi wa Hali halisi/Mazingira**

Kuhakikisha suala la usawa wa Kijinsia linapewa umuhimu wake katika kuangalia/kubaini uwezo, mapungufu fursa na changamoto za taasisi husika (SWOT Analysis). Kwa mfano, Je taarifa za Mchango wa NGOs na Sekta ya NGOs kwa ujumla katika maendeleo zinazingatia suala la usawa wa Kijinsia?

**(ii) Uchambuzi wa Wadau**

Kuhakikisha wanaume na wanawake wanashiriki. Endapo ni lazima kushirikisha Jinsia moja tu basi ni vizuri kueleza sababu za kufanya hivyo. – Changanua maoni ya wanaume na wanawake.

**(iii) Kupitia utendaji wa kila mwaka**

Kupitia Sera na mipango ya Taasisi husika na kubainisha masuala muhimu ya Kijinsia kama vile taarifa fursa n.k.

Pitia nyaraka mbalimbali za Taasisi husika ili kuona kama limetumia nyaraka muhimu kama MKUKUTA katika kujiwekea vipaumbale.

**(iv) Dira na Utume wa Shirika/Taasisi**

- Kuhakikisha kuwa vinachukua mtazamo wa Kijinsia
- Kupitia kuona kama malengo yaliyowekwa yana mtazamo wa Kijinsia.
- Kuangalia kama malengo yaliyowekwa yanatokana na uchambuzi wa Kijinsia.
- Kuangalia kama vipaumbele vilivyowekwa vimezingatia umuhimu wa Kijinsi katika Shirika.

(v) Kutoa ushauri/ kuandaa malengo mahususi yenye mtazamo wa Kijinsia yakionesha idadi ya wanawake na wanaume watakaonufaika au kushiriki. Aidha onesha namna watakavyoshiriki au kunufaika.

## 5.0 Umuhimu wa Bajeti na Kaguzi zenye Mtizamo wa Kijinsia

Bajeti yenye mtizamo wa Kijinsia ni ile ambayo inazingatia mahitaji na matakwa ya wanaume na wanawake, wavulana na wasichana katika jamii. Bajeti yenye mtazamo wa Kijinsia husaidia kufikia lengo la usawa Kijinsia. Bajeti yenye matizamo wa Kijinsia ndio husaidia kutekeleza malengo yaliyoanzishwa katika sehemu ya 4.0. Aidha, husaidia kufanya kaguzi zenye mtizamo wa Kijinsia.

# 6.0 Hitimisho

Katika mada hii nimejadili kuhusu uingizaji wa masuala ya Jinsia katika ufuatiliaji na tathmini za shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kufanya hivyo nimefafanua dhana ya Jinsia uingizaji wa masuala ya Jinsia na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Nimeeleza umuhimu na sababu za kuingiza masuala ya Jinsia kwenye tathmini ya shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; Hatua za kufuata katika uingizaji huo na umuhimu wa Bajeti na Kaguzi zenye mtazamo wa Kijinsia.

# 7.0 Mapendekezo

- Kupitia NGO Fomu Na. 10 na kuipa mtizamo wa Kijinsia.
- Kutoa mafunzo ya namna ya kuandaa Bajeti na kufanya Kaguzi zenye mtizamo wa Kijinsia kwa NGOs.

# ASANTE SANA KWA KUNISIKILIZA